TANGAZO La SERIKALI Na. 7 La Tarehe 13/1/2023

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,

(SURA YA 272*)*

---

# AMRI

---

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 28(d))*

AMRI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SONGEA ("SONGEA WSSA") YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama, Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea ("Songea WSSA") ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira), ya Mwaka 2023.

Marekebisho ya bei

2. Bei, ada na tozo za majisafi na usafi wa mazingira za Songea WSSA zinarekebishwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Masharti

3. Masharti yafuatayo yatatumika katika bei zilizoidhinishwa:

(a) kabla au ifikapo tarehe 31 Disemba 2023, Songea WSSA itawasilisha EWURA mpango wake wa biashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii;

(b) ndani ya miezi mitatu baada ya amri hii kutangazwa katika Gazeti la Serikali, Songea WSSA itawasilisha ushahidi EWURA kwamba imewajulisha wateja wake kuhusu amri hii pia imetoa elimu kwa wadau wake ikijumuisha wateja, viongozi wa serikali, viongozi wa siasa na wawakilishi wa taasisi za dini;

(c) Songea WSSA itaandaa na kutekeleza mpango

wa kuwafikia wateja kwa lengo la kuwaelimisha na kuwasilisha EWURA taarifa ya utekelezaji wa mpango huo kila mwaka;

(d) Songea WSSA itahakikisha deni lote la tozo ya udhibiti linalipwa ifikapo tarehe 31 Disemba 2023 na kuwasilisha kwa wakati tozo zote zinazokusanywa;

(e) Songea WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili;

(f) Songea WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu;

(g) Songea WSSA, kila mwaka na kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri hii; na

(h) Songea WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA na taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Songea WSSA ikilinganishwa na mamlaka nyingine za majisafi na usafi wa mazingira na uboreshaji wa huduma zake.

Kufutwa TS Na. 543 ya 2018

4. Amri ya Mamlaka ya MajiSafi na Usafi wa Mazingira Songea ("Songea WSSA") ya Kurekebisha Bei za Huduma za MajiSafi na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2018 inafutwa.

_____

JEDWALI LA KWANZA

_____

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa

| Kundi la Weja | Matumizi (m3) | Kipimo | Bei ya Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2021/2022 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 0-10 | Shilingi/m3 | 1,110 | 1,640 | 1,680 | 1730 |
| | 10<25 | | 1,200 | | | |
| | >25 | | 1,240 | | | |
| Taasisi | 0-20 | | 1,145 | 1,670 | 1,730 | 1,780 |
| | >25 | | 1,240 | | | |
| Biashara | 0-10 | | 1,240 | 1,720 | 1,770 | 1,820 |
| | >10 | | 1,330 | | | |
| Viwanda | 0-10 | | 1,240 | 1,720 | 1,770 | 1,820 |
| | >10 | | 1,330 | | | |
| Magati | | Shilingi/m3 | 500 | 1,000 | 1,000 | 1,000 |
| | | Shilingi/Lita 20 | 10 | 20 | 20 | 20 |
| Wastani | | Sh./m3 | 1,201 | 1,641 | 1,683 | 1,732 |

Jedwali Namba 1(b): Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Maunganisho Mapya ya Maji

| Kundi la Wateja | Ada ya sasa | Ada Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho kama ilivyoainishwa kwenye kanuni ya 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019 | Shilingi 26,000 | | |
| Taasisi | | | | |
| Biashara | | | | |
| Viwanda | | | | |

Jedwali Namba 1(c): Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 20,000 | 25,000 | 28,000 | 30,000 |
| Taasisi | 20,000 | 25,000 | 28,000 | 30,000 |
| Biashara | 20,000 | 25,000 | 28,000 | 30,000 |
| Viwanda | 20,000 | 25,000 | 28,000 | 30,000 |

Jedwali Namba 1(d): Tozo za Sasa na Zilizoidhinishwa za Uondoaji wa Majitaka kwa Gari la Songea WSSA (kwa tripu moja)

| Kundi la Wateja | Umbali (KM) | Tozo ya Sasa | Tozo Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Wateja Wote | 0-10 | 70,000 | 90,000 | 100,000 | 110,000 |
| | >10-20 | 80,000 | 100,000 | 110,000 | 120,000 |
| | >20 | 90,000 | 110,000 | 120,000 | 130,000 |

Jedwali Namba 1(e): Tozo za Sasa na Zilizoidhinishwa za Huduma ya Majitaka (TZS/$m^3$)

| Kundi la Wateja | Tozo ya Sasa | Tozo Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 400 | 480 | 480 | 480 |
| Taasisi | 650 | 780 | 780 | 780 |
| Biashara | 675 | 810 | 810 | 810 |
| Viwanda | 675 | 810 | 810 | 810 |

_____

JEDWALI LA PILI

_____

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(e))*

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

| Maelezo | | Gharama (TZS million) | | |
|---|---|---|---|---|
| Na | Mradi | 2022/2023 | 2023/2024 | 2024/2025 |
| 1 | Ununuzi na ufungaji wa pump mpya mbili zenye uwezo wa 486 mita za ujazo kwa saa kila moja katika kituo cha kusukuma cha Luhira . | 0 | 444.08 | 454.37 |
| 2 | Upanuzi wa mtandao wa majisafi kwa urefu wa kilomita 78 ifikapo Juni 2024/25 katika maeneo ya Luwawasi, Ruhuwiko, Subira, Seedfarm, Lizaboni, Tanga, Mjimwema, Sinai Namanditi na Mkuzo . | 193 | 183 | 173.1 |
| 3 | Ukarabati wa mtandao wa majisafi kwa kilomita 20 katika maeneo ya Lizaboni, Matarawe na Seedfarm | 155 | 155 | 158.7 |
| 4 | Ununuzi wa mita (dira) za malipo ya kablaya matumizi 600 zenye kipenyo cha milimita 20 | 74.93 | 74 | 75 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5 | Ununuzi wa mita (dira) 4320 za malipo ya baada ya matumizi zenye kipenyo cha milimita 15 | 121.87 | 125.29 | 158.81 |
| 6 | Ununuzi wa mashine tatu za kuwekea madawa ya kutibu maji | 24.6 | 24.6 | 24.74 |
| 7 | Ununuzi wa magari matatu | 75 | 76 | 98 |
| 8 | Ununuzi wa pikipiki 36 | 38 | 40 | 43 |
| 9 | Upanuzi wa mtandao wa majitaka kwa kilomita 7.5 katika maeaneo ya Majengo na Misufini | 45.03 | 46.38 | 47.77 |
| 10 | Ununuzi wa computa 50 na vifaa vya ICT ifikapo June 2025 | 77.59 | 81.84 | 85.77 |
| | Jumla ya uwekezaji | 805.02 | 1,250.19 | 1,319.26 |

_____

JEDWALI LA TATU

_____

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(f))*

VIASHIRIA VYA UTENDAJI

| Maelezo | Kizio | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Maunganisho Mapya ya Majisafi | No. | 1,440 | 1,440 | 1,440 |
| Maunganisho Mapya ya Huduma ya Majitaka | No. | 60 | 60 | 60 |
| Upotevu wa Maji | % | 19.5 | 19 | 18.5 |
| Kiwango cha Kufunga Dira za Maji kwa Wateja | % | 100 | 100 | 100 |
| Ufanisi katika Ukusanyaji wa Mapato | % | 92 | 95 | 95 |

Dodoma,
29 Desemba, 2022

MODESTUS M. LUMATO,
*Director General*